

## **THAMANI YA HESHIMA**

**Imefasiriwa na**

**Profesa Ayman Alasar**

**HOTUBA YA KWANZA.**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu: {**Hakika yako wewe Muhammad ni mwenye tabia nzuri zaidi**} na ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba sala salamu na baraka zimwendee Mtume Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi huo:**

Jambo la kushikamana na maadili mema pamoja na tabia njema ni katika misingi muhimu ya kusimama kwa dola na staarabu, na wala haiwezekani kujenga ustaarabu imara na wenyewe nguvu isipokuwa ni pindi maadili mema yanapokuwepo, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Mumekuwa nyinyi ni Uma bora ni kwa sababu**

**hutoka watu munaamrisha mema na kukataza maovu na munamuamini Mungu}.**

Jamii kushikamana na maadili mema na kuungana kwenye maadili hayo kuungana kwao kunaimarika zaidi kupitia kuheshimu misingi yake na kuifuata, kwani msemaji anasema:

*Kwa hakika Uma wenyе maadili mema umebakia - ikiwa maadili yao mema yataondoka basi na wao wataondoka.*

Hakuna shaka kuwa thamani ya heshima ni katika misingi mizuri ya ubinadamu ambayo imelinganiwa na Uislamu, na ambayo kila mwanadamu anatamani kunasibishwa nayo au kusifiwa nayo, kwani dini yetu imelingania kujipamba na thamani hii kwa sura zake zote, mionganoni mwake ni pamoja na kujiheshimu kwa mwanadamu kuchunga murua wake, na kuilinda nafsi yake na vitendo vinavyoleta aibu au lawala, hivyo anapaswa kujiweka mbali na maeneo ya riba na tuhuma, ambapo anasema Mtume Muhammad S.A.W “*Mwenye kujitenga na mambo ya tuhuma basi atakuwa ameitenga dini yake na heshima yake*” na anasema tena Mtume S.A.W “Haipaswi kwa Muumini kujidhililisha mwenyewe”.

Miongoni mwa misingi mwengine ni: Ni kuheshimu mwenye tafauti kidini kikabila na kitamaduni, kwa kuheshimu haki zake, kwani mtu mwengine wa tafauti ana haki ya kuheshimiwa mwili wake mali za na

anavyovimiliki, ambapo anasema Mola Mtukufu: {**Mwenyezi Mungu hawakatazeni wale ambao hawajapigana na nyinyi katika dini wala hawajawatoa majumbani kwenu kuwafanya wema na uadilifu kwani Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu}**} hili linaonekana wazi pale lilipopitishwa jeneza na Mtume S.A.W akasimama kutoa heshima ndipo Mtume alipoambiwa kuwa jeneza hilo aliyefariki na Myahudi! Mtume S.A.W akasema kwa kuuliza kuwa “*Je kwani si mwanadamu?*”

Miongoni mwa misingi mengine ni: Kumuheshimu mtu mkubwa kwa umri au kwa nafasi aliyonayo pamoja na kutambua ukubwa wake ambapo Mtume S.A.W anasema: “*Si katika sisi yule asiyemuheshimu mdogo wetu na kumuheshimu mkubwa wetu*”. Na anasema Mtume S.A.W “*Waweke watu kwenye nafasi zao*”, thamani hiyo imeonekana wazi pale Mtume S.A.W alipoamrisha Maswahaba R.A kusimama kumpa heshima Saad Ibn Muadh R.A na akawaambia “*Simameni kwa ajili ya kiongozi wetu*”. Na akasema Omar Ibn Khattab R.A Abubakri ni kiongozi wetu na alimwacha huru kiongozi wetu kwa maana ya kumwacha huru Bilali R.A, na pindi Mtume S.W.A alipouliwa kuhusu mti mfano wake ni kama vile Muislamu kwani unatoka matunda yake kila wakati kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu, jani lake wala halidondoki, na imetokea kwa Swahaba Abdillah Ibn Omar R.A kuwa ni kama mtende kwa maana ya kuwa na faida kwa kila pande, kwani majibu yake

yalikuwa ni sahihi, lakini pamoja na umri wake ni mdogo lakini alichukia sana kumjibu Mtume S.A.W mbele ya Maswahaba wakubwa Abibakri na Omar kwa kuwaheshimu, pamoja na Maswahaba wengine wakubwa *Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe kwao.*

### **Hotuba ya Pili.**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mlezi wa walimwengu wote, swala na salamu zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Miongoni mwa sura nzuri za heshima ni pamoja na kumuheshimu mwalimu na kunyenyekea kwake, pamoja na kutekeleza haki zake hasa kwakuwa Uislamu umeinua nafasi yake na heshima yake, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu amelinganisha ushuhuda wake na ushuhuda wa Malaika kwa ushahuda wa Wanachuoni na akasema Mola Mtukufu: {**Mwenyezi Mungu, na Malaika, na wenyewe elimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana mungu ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu, hapana mungu ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hekima**}.

Na Anasema tena Mola Mtukufu: {**Mwenyezi Mungu huwainua daraja wale walioamini miongoni mwenu na wale waliopewa elimu**}.

Na anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W “*Mtu mwenye elimu*

*huombewa msamaha na waliomo mbinguni na ardhini pamoja na papa baharini, na ubora wa Mwanachuoni kwa asiyekuwa Mwanachuoni ni kama ubora wa mwezi wa usiku wa badri dhidi ya sayari zengine, kwa hakika Wanachuoni ni warithi wa Mitume”.*

Haja yetu kubwa ni kuenea kwa thamani ya heshima ndani ya jamii zetu, na kubadilika kuwa utamaduni wanaouishi wadogo na wakubwa mwanamme na mwanamke na kuleta uhai katika jamii na kuinua thamani ya jamii mpaka mshikamano uenee kwa wote pamoja na ustawi maendeleo na utulivu.

**Tunakuomba Mwenyezi Mungu utuongoze kwenye maadili mema na  
uhifadhi nchi yetu na nchi zengine za ulimwengu wa Kiarabu na  
Kiislamu.**